

Sportpesa mwatufilisi!

Naikata ya kalima, kufunua ya moyoni,
Kidede ninasimama, kuwambia hadharani,
Kwetu nyinyi mwatuchuma, mwatuwacha maskini,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Mwataka tuishi vipi, kiturai kwazo timu?
Mwatunasa kwa makapi, bila ya zetu fahamu,
Tukisha weka mabeti, nyoyoni mwatabasamu,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Pale chini huandikwa, 'maximum' wini ya laki,
Kumbe hayo ni kupakwa, mafuta kwao mswaki,
Kingoja uje kuvikwa, keshanyonywa yako steki,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Nanywa maji kwa sukuma, hela zangu kiekeza,
Sili ugali mlima, yangu mia nawekeza,
Kijashinda nikavuma, hizo hela naziwaza,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Hili pepo la jackpot, mekuwa nduli jamani,
Ndoto zingine si oti, nona jackpot mfukoni,
Hata kobole ya switi, elitebet mwao kinywani,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Sportpesa mwatufilisi, mebakia kuwa hoi,
Mekuwa kama mafisi, twalia hata wa Voi,
Kakwisha zetu nakisi, hatwezi hata jidai,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Vyuoni mote dunia, mwatula tukiwa hai,
Kiweka dau la mia, hela nyangi mwaturai,
Kinyume pale hujia, ukabaki kuwa hoi,
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

Likizo najipatia, tarudi bada ya wiki,
Mwenzenu nenda tulia, yangu simu siishiki,
Nimeliwa najilia, sportpesa hamridhiki!
Mwatufilisi sportpesa, mwataka tuishi vipi?

*Savonge Peter,
Malenga wa Nchi Kavu,
Chuo Kikuu cha SEKU-Kitui.*